

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
6 Julai 2008**

Waliohudhuria

Ally Athuman Jumbe
Ally Saidi Mwishehe
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Husein Hamza Hamisi
Juma Ali Salehe Jonggo
Juma Hassan Chibaya

Mradi wa Usalama Barabarani - Wamba Memorial Fund

Elaine alichapa manual ya kiswahili, bila picha, na Filbert alisema atapitia kusahihisha. Elaine ataweka picha ndani.

Wakati wa wiki Juma alienda ofisini kwa bwana Wamba wa Chuo cha Usafirishaji, na pia Elaine aliongea naye kwa simu. Alisema kwamba booking ya darasa ipo tayari kwa wiki 21-26 July. Alipendelea tuende kumwona wiki hii kuongea kuhusu vipi Chuo cha usafirishaji watashiriki katika training.

Elaine alipiga simu shule ya Mbondole kualika mwakilishi mmoja na walisema watamwambia nani atahudhuria baadaye. Atapiga simu kwa Kigamboni Secondary School wiki hii. HUWATA walisema kwa simu kwamba watampa Juma orodha ya wawakilishi wao wiki hii.

Juma alipata orodha ya bei ya Mama Lishe anaitwa Mama Alex (0717205157) ambaye yupo nje ya chuo. Tsh 2,000 kwa mtu kwa siku itatosha kwa chai ya asubuhi na chakula cha mchana.

Elaine alimtumia email kwa Andrew kumwuliza kama atapenda kutembelea TANROADS na Mama Mlamba wakati yupo Dar es Salaam. Ataandika barua ya kuomba appointment. Juma alisema ofisi ya Mama Mlamba imehamia Ubungo plaza.

Ofisi

Mejah bado hajapaka rangi kwenye ofisi mpya.

Kodi ya TRA

Juma alimpa Mama Mlamba wa serekali ya jiji na Bwana Ngaja wa kampuni nakala ya barua tuliyopokea kutoka TRA.

Mambo ya hela

Wakati wa wiki Juma alimpa Juma Chibaya Tsh 1,000 kwa ajili ya dawa ya paa ya ofisi mpya na alitumia Tsh 300 kwa ajili ya photocopy ya barua ya TRA. Ally Saidi Mwishehe alitumia Tsh 6,000 kununua mpria mpya ya guta na alimpa Juma Tsh 8,000 (Tsh 14,000 toa Tsh 6000) kwa kodi ya guta ya wiki mbili. Sasa Juma anabaki na Tsh 68,900 ya hela ya UWABA.

Document ya guta

Robert Bartlett aliandaa document kuhusu maguta kwa kutumia video Markus aliyemtumia, na alitutumia kwa email.